

Yesu Kristo Ni Nani? (Sehemu ya 2)

Inategemea sura ya 4 ya kitabu *Biblia Inafundisha Nini Hasa?* kinachopatikana kwenye Tovuti ya jw.org/sw.

LENGO: Chunguza mambo unayoamini na sababu za kuamini mambo hayo, chunguza kile ambacho Biblia inafundisha, na uone jinsi unavyoweza kuwaeleza wengine mambo unayoamini.



JE, YESU YUKO SAWA NA MUNGU?

1 CHUNGUZA MAMBO UNAYOAMINI

Kwa nini huenda watu wengine wakasema ndiyo?

Kwa nini huenda watu wengine wakasema hapana?

Wewe unaamini nini?

Kwa nini unaamini hivyo?

2

CHUNGUZA BIBLIA INAFUNDISHA NINI

Yesu alikuwa na mwanzo; Mungu hana mwanzo.

(Tazama sura ya 4 ya kitabu *Biblia Inafundisha*, fungu la 10-12.)

Soma Wakolosai 1:15, 16.

Kwa nini Biblia inamwita Yesu “mzaliwa wa kwanza wa *viumbe vyote*”?

Soma Zaburi 90:2.

Je, Yehova Mungu alikuwa na mwanzo?



Ikiwa Yesu yuko sawa na Mungu, kwa nini alimwita Mungu Baba, na si ndugu?

Yesu alifundisha kwamba Mungu ni mkuu kuliko yeye.

(Tazama sura ya 4 ya kitabu *Biblia Inafundisha*, fungu la 12-14.)

Soma Yohana 14:28.

Kulingana na andiko hilo, je, Yesu alijiona kuwa sawa na Mungu?

Soma Yohana 14:31.

Kwa kukubali kutii amri za Mungu, Yesu alionyeshaje kwamba yeye si sawa na Mungu?

Ni nini kinachokusadikishia kwamba Yesu si Mungu?

3

ELEZA MAMBO UNAYOAMINI

MTU AKISEMA . . .

Yesu alishuka kutoka mbinguni, hivyo yeye ni Mungu.

UNAWENZA KUMJIBU HIVI . . .

Ni kweli kwamba Yesu aliishi mbinguni kabla ya kuja duniani. Lakini siamini kwamba hilo linamfanya kuwa sawa na Mungu kwa sababu . . .

Unaweza kumwonyesha mtu huyo andiko gani?

Ukizingatia maoni yake, unaweza kuelezaje andiko hilo kwa njia yenye kusadikisha?

MTU AKISEMA . . .

Yesu alisema kwamba yeye ni Mungu.

UNAWENZA KUMJIBU HIVI . . .

Huenda watu wengi wakakubaliana nawe. Lakini ninaamini jambo tofauti kwa sababu . . .

Unaweza kumwonyesha mtu huyo andiko gani?

Ukizingatia maoni yake, unaweza kuelezaje andiko hilo kwa njia yenye kusadikisha?
